



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU

**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA
DAWA ZA KULEVYA**



TAARIFA KWA UMMA

LITA 66,048 ZA KEMIKALI BASHIRIFU ZAKAMATWA DAR ES SALAAM

Dar es Salaam, Mei 13, 2026.

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania, mwezi Aprili 2026 ilifanya operesheni maalum jijini Dar es Salaam na kufanikiwa kukamata jumla ya lita 66,048 za kemikali bashirifu zilizoingizwa nchini kinyume na taratibu za kisheria.

Kemikali zilizokamatwa ni Cyclohexanone zenye ujazo wa lita 16,048 pamoja na Extra Neutral Alcohol (ENA) zenye ujazo wa lita 50,000. Aidha, magari mawili yaliyohusika katika usafirishaji wa kemikali hizo yanashikiliwa na watuhumiwa wawili wamekamatwa kuhusiana na tukio hilo.

Kutokana na udhibiti wa dawa za kulevya kuimarika duniani, mitandao ya kihalifu imekuwa ikitumia kemikali bashirifu kuzalisha dawa za kulevya katika maabara bubu. Kemikali hizo ni halali kwa matumizi mbalimbali ya viwandani, kitabibu, kilimo, ujenzi, madini pamoja na tafiti za kisayansi, lakini wahalifu huzitumia vibaya kwa kuzichepusha kutoka katika matumizi halali na kuzitumia kutengeneza dawa za kulevya.

Hali hiyo imeongeza changamoto katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya duniani na kuifanya nchi yetu kuendelea kuimarisha mifumo ya udhibiti wa kemikali bashirifu ili kuzuia uchepushwaji wake katika matumizi haramu.

Uchunguzi uliofanyika umebaini kuwa, kemikali aina ya Cyclohexanone ziliingizwa nchini na kampuni ya Kinglion Investment Company LTD kinyume na matakwa ya mifumo ya udhibiti ikiwemo kibali kutoka Mamlaka husika.

Aidha, kemikali aina ya Extra Neutral Alcohol (ENA) zilikuwa zinasafirishwa kwa kutumia magari yanayotumika kubeba mafuta ya nishati yaliyoandikwa *Danger Petroleum 3YE 1203* kwa kutumia vibali vya kughushi. Magari hayo aina ya Scania yalikuwa yakibeba kemikali kutoka kampuni ya Maranile Group Company Limited iliyopo Kibaha Mkoa wa Pwani.

Katika operesheni hiyo, Mamlaka ilimkamata Bakira Abel Zacharia (44), mkazi wa Dar es Salaam, dereva wa gari namba T 794 BMB lenye tela tanki namba T 166 AHW lililokuwa limebeba lita 30,000 za kemikali hizo.

Pia, alikamatwa Vicent Stephen Rashid (26), mkazi wa Mbeya, dereva wa gari namba T 568 EQF lenye tela tanki namba T 640 EQN lililokuwa limebeba lita 20,000 za kemikali hizo.

Mazingira ya uingizaji na usafirishaji wa kemikali hizo yanaashiria uwepo wa nia ovyo ya kuzichepusha kwa matumizi haramu, ikiwemo utengenezaji wa dawa za kulevyo. Kemikali aina ya Cyclohexanone ni miongoni mwa kemikali zinazodhibitiwa kimataifa kutokana na taarifa za kutumika katika maabara bubu zinazozalisha dawa za kulevyo aina ya Phencyclidine (PCP).

Aidha, Lita 16,048 za kemikali za Cyclohexanone zilizokamatwa kama zingechepushwa, zingeweza kuzalisha Tani 11.4 za dawa za kulevyo aina ya Phencyclidine kwa kuwa kilo moja ya kemikali hizo huweza kuzalisha takribani gramu 750 za dawa za kulevyo.

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani Sura 182, usafirishaji wa kemikali unahitaji kufuata taratibu maalum ikiwemo kuwa na vibali vya kuingiza na kusafirisha. Matumizi ya vibali vya kughushi pamoja na utoaji wa taarifa za uongo kuhusu matumizi yaliyokusudiwa ya kemikali husika ni kosa kisheria.

Aidha, usafirishaji wa kemikali kwa njia fiche hususani kwa kutumia magari ya kubeba Petroli ni ukiukwaji wa taratibu za udhibiti wa kemikali na ni kiashiria cha uwepo wa jaribio la kuzichepusha kwa matumizi haramu ikiwemo utengenezaji wa dawa za kulevyo.

Kwa upande wa dawa za kulevya, Mamlaka ilifanya operesheni katika mikoa ya Dodoma, Mtwara, Njombe, Ruvuma, Kilimanjaro, Arusha, Dar es Salaam, Morogoro na Mwanza na kukamata bangi tani 5.733, mirungi tani 1.67, heroin gram 48.23, cocaine gramu 113.35 na kuteketeza ekari 38.5 za mashamba ya bangi. Aidha, magari manne (04) pamoja na pikipiki 14 zilizohusishwa na biashara hiyo haramu zilikamatwa huku watuhumiwa 84 walikamatwa kusuana na ukamataji huo.

Mamlaka itaendelea kushirikiana na taasisi za kitaifa na kimataifa kuimarisha udhibiti wa kemikali bashirifu zinazoweza kutumika katika utengenezaji wa dawa za kulevya. Hivyo, wadau wote wa kemikali wanapaswa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa. Kinyume na hapo, hatua kali za kisheria zitaendelea kuchukuliwa dhidi ya wote watakaobainika kujihusisha na vitendo hivyo.

Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, inawasihi wananchi kuendelea kutoa taarifa za vitendo vinavyohusiana na dawa za kulevya pamoja na uchepushaji wa kemikali bashirifu ili kusaidia juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya.

Imetolewa na;

Joachim

Kitengo cha Mawasiliano ya Serikali
**MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA
NA DAWA ZA KULEVYA.**